

A woman with dark hair is shown in a close-up, looking down with a distressed expression. Her right hand is raised to her forehead, with fingers spread, suggesting she is covering her eyes or feeling overwhelmed. The background is dark and out of focus.

***Wasiwasi,
msongo &
dukuduku***

MATHAYO 6

25. "Ndiyo maana nawaambieni, msiwe na wasiwasi juu ya chakula na kinywaji mnavyohitaji ili kuishi, wala juu ya mavazi mnayohitaji kwa ajili ya miili yenu. Je, maisha ni chakula tu au zaidi? Na mwili, je, si zaidi ya mavazi?"
26. Waangalieni ndege wa mwituni: hawapandi, hawavuni, wala hawana ghala yoyote. Hata hivyo Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je, nyinyi si wa thamani kuliko hao?"
27. Ni nani miongoni mwenu kwa kuwa na wasiwasi sana anaweza kuuongeza muda wa maisha yake?"

MATHAYO 6

28. "Na kuhusu mavazi, ya nini kuwa na wasiwasi?
Tazameni maua ya porini jinsi yanavyostawi.
Hayafanyi kazi wala hayasokoti.
29. Lakini nawaambieni, hata Solomoni mwenyewe
na fahari zake zote hakupata kuvikwa vizuri
kama ua mojawapo.
30. Ikiwa basi, Mungu hulivika hivyo jani la
shambani ambalo leo liko na kesho latupwa
motoni, je, si atawafanyia nyinyi zaidi? Enyi
watu wenye imani haba!

MATHAYO 6

31. "Basi, msiwe na wasiwasi: 'Tutakula nini, tutakunywa nini, tutavaa nini!'

32. Maana hayo yote yanahangaikiwa na watu wasiomjua Mungu. Baba yenu wa mbinguni anajua kwamba mnahitaji vitu hivyo vyote.

33. Bali, shughulikeni kwanza juu ya ufalme wa Mungu na matakwa yake, na hayo yote mtapewa kwa ziada.

34. Basi, msiwe na wasiwasi juu ya kesho; kesho inayo yake. Matatizo ya siku moja yanawatosheni kwa siku hiyo."

WASIWASI NA DUKUDUKU

- Wasiwasi, dukuduku na msongo unasababishwa na mwitikio wetu kwa vitisho kihisia au kimwili, viwe halisi au vya kufikirika.
- Itakuwaje nikitekwa nyara? Itakuwaje mke wangu akiniacha? Nitalipaje bili mwezi huu? Je, kutakuwa na mashambulizi zaidi ya kigaidi? Vipi kuhusu hali ya kisiasa katika nchi? Itakuwaje nikipoteza kazi yangu? Vipi kama ongezeko la joto duniani kuongezeka? Itakuwaje tukitumia mafuta yote? Ni cholesterol yangu kubwa mno? Itakuwaje nikifeli mitihani?

Kuwa na wasiwasi juu ya kitu ambacho kinatarajiwa kutokea na hakitokea - ni mateso kwa ajili ya kitu ambacho hakitatokea kamwe. ¹

¹ <http://christianlives.org/sermons/ANXIETY86.doc>

Madhara

ya

msongo



KUKOSA RAHA

- ❑ Methali 12:25 Wasiwasi moyoni humkosesha mtu raha, lakini neno jema humchangamsha.
- ❑ Cha kushangaza ni kwamba neno 'worry' (wasiwasi) chimbuko lake ni katika neno la zamani la Kiingereza 'wyrgran' na maana yake ni 'to stragle' (kunyonga). Neno hilo lilifuatiwa na neno 'worien' ambalo lilileta maana zaidi ambayo ni "kukamata shingo katika koo kwa kutumia meno na kurarua." ¹
- ❑ Arthur Somers Roche alisema, "Wasiwasi ni mkondo mwembamba wa hofu unaotiririka akilini, na endapo utaendekezwa, huunda mfereji ambao utakausha mawazo yote."



¹ CHANZO: <http://www.thefreedictionary.com>

KUKOSA RAHA

- ❑ Mwandishi, malenga na waziri wa Kikristo George MacDonald alisema, "Si mawazo kuhusu leo bali mawazo kuhusu kesho ndiyo humwangusha binadamu."
- ❑ "Wasiwasi haufuti huzuni za kesho lakini hufuta furaha ya leo." (Leo Buscaglia)
- ❑ "Mara nyingi wasiwasi hukipa kitu kidogo kivuli kikubwa." (Methali ya Kiswidi)
- ❑ "Si kazi ambayo huchosha, bali wasiwasi." (Methali ya Kiafrika)

**Huwa nashikwa
na msongo wa
mawazo mara
mbili**



usiku na Mchana

KUKOSA RAHA

- ❑ Wasiwasi na msongo hutudhuru kiakili, kihisia na kimwili. Dalili ya msongo wa mawazo ni kuchoka sana, kuumwa kichwa, misuli kuvuta, kupumua kwa kasi, kutetemeka, umakini mdogo na kutegemea zaidi wengine.
- ❑ Ishara zingine ni kushindwa kupumzika, kuwa mpweke, kujitenga, maumivu na kuumwa, kuharisha au kuvimbiwa, kichefuchefu, kulala sana au kidogo na matumizi ya madawa ya kulevya.¹

¹ SOURCE: Wikipedia - Stress (biology)

HUKUI KIROHO

- ❑ Wasiwasi hautudhuru kiakili, kihisia na kimwili tu - hutudhuru kiroho pia.
- ❑ Kwa sababu wasiwasi hutupotezea muda na kutukatisha tamaa, hutuzuia kukua kiroho - hivyo tunabaki wadogo kiroho.
 - Luka 8:14 Zile zilizoanguka kwenye miti ya miiba ni watu wale wanaosikia lile neno, lakini muda si muda, wanapokwenda zao, husongwa na wasiwasi, mali na anasa za maisha, na hawazai matunda yakakomaa.



KIZUIZI CHA NJIA YETU KWA MUNGU

- Luka 10:39-42 ... Maria... aliketi karibu na Yesu akisikiliza mafundisho yake. Lakini Martha anashugulika na mambo mengi. Basi akamwendea Yesu, akamwambia, "Bwana, hivi hujali kwamba dada yangu ameniacha nishughulike peke yangu? Mwambie basi anisaidie." Lakini Bwana akamjibu, "Martha, Martha, unahangaika na kusumbuka na mambo mengi. Kitu kimoja tu ni muhimu. Maria amechagua kitu bora zaidi ambacho hakuna mtu atakayemnyang'anya."



KUTOKUA MWANGALIFU

- Luka 21:34 "Muwe macho, mioyo yenu isije ikalemewa na anasa, ulevi na shughuli za maisha haya. La sivyo, siku ile itawajieni ghafla. Kwa maana itawajia kama mtego wote wanaoishi duniani pote."
- Kama tunataka kuwa tayari mpaka kurudi kwake Yesu. Tunaambiwa tusiwaze sana kuhusu maisha.



***Chanzo cha
msongo***




WASIWASI & DUKUDUKU

- Yesu ametupatia mifano mitatu (3) ya vitu vya kawaida:
 - 1) Chakula (mahitaji muhimu)
 - 2) Nguo (mitindo)
 - 3) Maisha Marefu (afya)
- Mwandishi na mhubiri maarufu wa injili John McArthur ameandika, "Mungu hutambua kwamba binadamu, katika tamaa yake, katika maisha yake yote huwa anajishughulisha kujali vitu vya nje - chakula chake, nyumba yake, mavazi yake n.k ." ¹

¹ Overcoming Materialism - Overcoming Financial Worry - Part 1 by John McArthur

(<http://www.biblebb.com/files/mac/sg2248.htm>)



John McArthur

1) MAHITAJI MUHIMU

- ❑ Mathayo 6:25 Ndiyo maana nawaambieni, msiwe na wasiwasi juu ya chakula na kinywaji...
- ❑ Tunaweza kufikiri kwamba ni sawa kutilia shaka mahitaji yetu na sio tamaa zetu. Lakini Yesu anatufundisha kwamba hata hilo huonesha ukosefu wa imani kwa upande wetu wakati Baba yetu wa mbinguni huweza kutupatia.
- Zaburi 37:25-26 Nilikuwa kijana sasa ni mzee; kamwe sijaona mwadilifu ameachwa na Mungu, au watoto wake wakiombaomba chakula. Daima yu radhi kukopesha, na watoto wake ni baraka.



KUTHAMINI PESA NA MALI

- ❑ Ni kweli, katika jamii yetu ya magharibi watu wengi wanayo mahitaji muhimu lakini bado wanataka kukusanya mali na ulaji. Kisha huwa na wasiwasi juu ya jinsi ya kulipa deni walilokusanya na jinsi ya kulinda mali zao na uwekezaji wao.
 - Watu wengi huingia katika madeni kwa kujaribu kujihusisha na watu ambao tayari wana madeni.
- ❑ Baadhi ya watu wana vyote wanavyohitaji na bado wana wasiwasi kuhusu siku zijazo. Hivyo kwa sababu ya hofu yao dhidi ya baadaye hujaribu kuamua hatima yao wenyewe mbali na Mungu.
 - Mhubiri 5:12 Usingizi wa kibarua ni mtamu, awe ameshiba au amekula kidogo tu. Lakini usingizi wa tajiri ni wasiwasi daima, maana ziada ya mali yake humsumbua usiku kucha.

2) MTINDO

- Mathayo 6:28 "Na kuhusu mavazi, ya nini kuwa na wasiwasi?"
 - Katika baadhi ya jamii, watu masikini huweza kuwa na wasiwasi juu ya kutokua na mavazi au viatu.
 - Katika jamii yetu ya magharibi ambako watu wengi wana mavazi mengi, watu hujali zaidi kama mavazi yao yapo katiko mtindo au mwenendo wa kisasa, watu wana mtazamo wa kidunia kuhusu mavazi.



2) MTINDO

- ❑ Tumejifanyia mungu wa mitindo, sisi hujiingiza katika manunuzi ya mavazi ambayo hatuyahitaji mara kwa mara. Mara nyingi kinachonunuliwa huvaliwa mara moja au mbili kabla hakijafifia na kutohitajika tena.
- ❑ Tunatumia nguvu na muda mwingi kujaribu kuwa katika mtindo. Na mitindo huendelea kubadilika kila mara, hivyo huchochea manunuzi na ulaji zaidi.




2) MTINDO

- ❑ Tanataka kuonekana vizuri kwa sababu ya hofu jinsi watu wanavyotufikiria. Hofu yetu nyingi huweza kuonekana pia katika kumwogopa (hofu ya) mtu.
 - Kuwaogopa watu ni kujitega mwenyewe. (Methali 29:25)
 - 'Mwenyezi-Mungu ni ngome ya maisha yangu, sitamwogopa mtu yeyote. (Zaburi 27:1)
 - Namtumainia Mungu, wala siogopi. Binadamu dhaifu atanifanya nini? (Zaburi 56:4)
- ❑ Watu wangeacha kujali jinsi watu wengine wanavyowafikiria kama wangepahamu jinsi nadra wanavyofikiriwa. Hawakufikirii - maana hata wao huwaza wewe hufikiria nini juu yao. ¹

¹ <http://junialeigh.wordpress.com/2010/06/07>

3) AFYA & MAISHA MAREFU

- ❑ Watu hupenda kuishi maisha marefu. Hivyo hupata vitamini, kula chakula muhimu na kufanya mazoezi.
- ❑ Hutakiwi kutilia shaka maisha marefu.
 - Mathayo 6:27 Ni nani miongoni mwenu kwa kuwa wasiwasi sana anaweza kuongeza muda wa maisha yake?
- ❑ Sio tu kushindwa kurefusha maisha yako kwa kuwa na wasiwasi, lakini utayafupisha pia. Magonjwa mengi na vifo kabla ya wakati husababishwa na mfadhaiko na msongo.





***Kwa nini
wasiwasi?***



WASIWASI HAUNA FAIDA

- Malenga wa Kiingereza John Dryden alisema, "Binadamu huzuia furaha yake kwa mawazo ya kwamba itakuwaje?"
- "Wasiwasi ni maslahi ya kulipwa juu ya shida kabla haijatokea. (William Ralph Inge)

Vitu vingi nilivyotilia shaka
havijawahi kutokea.

WASIWASI HAUNA FAIDA

- Matatizo ambayo hutusababishia msongo wa mawazo - yanaweza kuwa ya ukweli au ya kufikirika - lakini madhara ni yaleyale:
 - “Kiasi gani cha maumivu walichotugharimu, maovu ambayo kamwe hayakutokea.” (Rais wa Marekani Thomas Jefferson)
 - Mcheshi wa Kimarekani Josh Billings alisema, “Kuna watu ambao hutarajia shida, hivyo hupitia huzuni ambazo hazijawahi kuwakuta.”

WASIWASI HAUNA FAIDA

- ❑ Wasiwasi ni kama kiti cha bembea, unajishughulisha nacho lakini hakikupeleki kokote.
- ❑ Kama tukiwa na wasiwasi kuhusu kesho na leo, hofu yetu hutambulika, tumekuwa na wasiwasi mara mbili! Kama hatutapangilia mawazo yetu, tutakuwa tumeshikwa na wasiwasi wa bure.¹

¹ <http://christianlives.org/sermons/ANXIETY86.doc>

WASIWASI HAUNA FAIDA

- Yesu anatufundisha kwamba wasiwasi hauna faida na haufanikishi chochote katika kutatua matatizo (mfano: afya na maisha marefu)
 - "Ni nani miongoni mwenu kwa kuwa na wasiwasi sana anaweza kuuongeza muda wa maisha yake?" (Mathayo 6:27)

"Wasiwasi ni kupoteza muda wa leo na kuvuruga mipango ya kesho kwa shida za jana." (William Ward)



HUKUFANYA USIZAE MATUNDA

- Yesu alisema, "Ile mbegu iliyoanguka kati ya miti ya miiba, ni mfano wa mtu asikiaye hilo neno, lakini wasiwasi wa ulimwengu huu na anasa za mali hulisonga neno hilo, naye hazai matunda." (Mathayo 13:22)
 - Katika hadithi hii, ile mbegu huwakilisha mbegu ambayo kamwe haizai- hakukuwa na uzao au mavuno ya kiroho. (Tofauti na mbegu nzuri.)



**Kama unataka usiwe na upungufu kiroho
- acha kuwa na wasiwasi na dukuduku.**

WASIWASI NI IMANI POTOFU

- ❑ Wasiwasi na hofu huandama imani yako - kwamba vitu havitofanikiwa.
 - “Wasiwasi ni imani hasi, kuamini visivyofurahisha, kujihakikishia majanga na kuamini kushindwa.” (William Ward)
- ❑ Hofu huonesha upungufu wa imani.
 - Wakati wa dhoruba ziwani, Yesu aliwaambia wafuasi wake “Enyi watu wenye imani haba; mbona mnaogopa?” (Mathayo 8:26)
 - Katika habari ya wasiwasi juu ya mavazi Yesu anasema, “Ikiwa basi, Mungu hulivika hivyo jani la shambani... je, si atawafanyia nyinyi zaidi? Enyi watu wenye imani haba?”



***Njia ya Biblia
kukabiliiana
na
msongo***

MBADALA WA BIBLIA

- Yesu anatufundisha njia 3 za kukabiliana na wasiwasi na msongo wa mawazo.
 - 1) Kumbuka una Baba wa mbinguni, hivyo, kuwa na imani naye na fikisha matatizo yako kwake kwa njia ya maombi.
 - 2) Angalia jinsi unavyothamini vitu. Pata mtazamo wa Kimungu juu ya pesa na mali, afya na mahitaji muhimu.
 - 3) Ishi leo - usijiongezee mzigo kwa kutarajia matatizo ya siku za baadaye.

1) BABA WA MBINGUNI

- Hutakiwi kuwa na wasiwasi juu ya fedha na mahitaji ya maisha (utakachokula, utakachokunywa au utakachovaa) ukimtambua Baba yako ni nani. Watoto wangu hawana wasiwasi kuhusu mlo wao ujao utapatikana wapi. Hawana wasiwasi kama watapata mahala pa kuishi au mavazi. Mawazo hayo hayapiti vichwani mwao kwa sababu wanajua baba yao atawapatia. Hata hivyo, bado sisi hatuamini kama Baba yetu wa mbinguni atatupatia.
- Mathayo 7:9-11 "Je, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye mtoto wake akimwomba mkate, atampa jiwe? Au je, akimwomba samaki, atampa nyoka? Kama basi nyinyi, ingawa ni waovu, mwajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, hakika, Baba yenu wa mbinguni atafanya zaidi: atawapa mema wale wanaomwomba."

1) BABA WA MBINGUNI

- ❑ Mathayo 6:26 Waangalieni ndege wa mwituni: hawapandi, hawavuni wala hawana ghala yoyote. Hata hivyo Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je, nyinyi si wa thamani kuliko hao?
- ❑ Je, mbwa wako huwa na wasiwasi juu ya mlo wake ujao kwa sababu ya hali ya uchumi?
 - Ndege hawakutani pamoja na kusema "Tunatakiwa tuweke mpango wa kutuwezesha kuishi." ... Lakini Mungu ameweka kitu ndani ya ndege nao hufanya vitu bila kufundishwa, wana nguvu ya ajabu ya kutafuta vitu muhimu kwa kuishi. Mungu haundi maisha tu, bali huyaendeleza pia. ¹



¹ Overcoming Materialism - Overcoming Financial Worry - Part 1 by John McArthur (<http://www.biblebb.com/files/mac/sg2248.htm>)

1) BABA WA MBINGUNI

- Jambo hili lisikaribishe uvivu, usiseme kwamba, "sitofanya kazi, kwani Mungu atanipatia chakula" Ujue kwamba anga haliwanyeshei ndege chakula chao, Mungu huwalisha ndege kwa kuwapa utambuzi ambao huwaonesha wapi pa kupata chakula na kukifanyia kazi. Hujishughulisha na kutafuta, hula wadudu wadogo, huandaa viota vyao, hutunza vifaranga vyao, huwafundisha jinsi ya kuruka... kazi yote hii itafanyika kama watakula... ¹
- Mwanzo 3:17-19 "Kwa hiyo, kwa kosa lako ardhi imelaaniwa... Kwa jasho utajipatia humo riziki yako, siku zote za maisha yako..."
- 2 Wathesalonike 3:10 Tulipokuwa pamoja nanyi tulikuwa tukiwaambieni, "Mtu yeyote asiyependa kufanya kazi, asile chakula."

¹ Ibid

1) BABA WA MBINGUNI

□ ... na bado wao wanafanya hivyo kwa utambuzi na hawafanyi zaidi. Hawasemi, "Nitajenga kiota kikubwa. Nitaweka wadudu wengi zaidi." wanafanya kazi kwa kiwango ambacho Mungu amewawekea na hawajiingizi sana katika shughuli hizo. Ndege hunenepa tu pale anapowekwa na binadamu katika banda. ¹

□ Binadamu ndiye kiumbe mwenye kila kitu anacho hitaji lakini bado hufikiria kulimbikiza na kujiwekea akiba. Wanapuuzwa ahadi na vipaumbele vya Mungu. Ndege hawana wasiwasi watapata wapi chakula, wao huruka mpaka watakapo kipata... na Mungu huwapa. Ndege hawana sababu ya kuwa na wasiwasi, na kama wao hawana sababu, wewe wasiwasi wako ni nini?



¹ Ibid

1) BABA WA MBINGUNI

- Tutawasiliana vipi na Baba yetu wa mbinguni endapo tutakumbwa na dukuduku?
 - a) Sala - wasilisha maombi yako kwa Mungu.
 - b) Imani - Amini kwamba Baba yako atakamilisha maombi yako.
 - c) Sifu - kwa imani, sifu jibu la Mungu kwako.
 - d) Nyenyekesa - kama mtoto mwadilifu, kubali kuwa chini ya madaraka ya Mungu bila kujali ni jibu gani amekupa.

(a) Sala

- Usiwe na wasiwasi - sali
 - "Msiwe na wasiwasi juu ya kitu chochote, ila kwa kila hali, mwombeni Mungu katika sala juu ya mahtaji yenu, kwa shukrani. Nayo amani ya Mungu ipitayo akili zote za watu italinda salama mioyo na akili zenu katika kuungana na Kristo Yesu" (Wafilipi 4:6-7).
 - "Nilimwomba Mwenyezi-Mungu naye akanijibu, na kuniondoa katika hofu zangu zote" (Zaburi 34:4).
- "Usiogope kuiamini kesho isiyojulikana kwa Mungu anayejulikana." (Corrie ten Boom)



(a) Sala

- ❑ Yakobo 5:13 Je, pana mtu yeyote miongoni mwenu aliye na shida? Anapaswa kusali.
- ❑ Kama unamuamini Mungu, na kwamba anakupenda na atatimiza malengo yako, basi tulia na kuwa na imani. Endapo kwa sababu yoyote ile ukadhani kwamba Mungu hatakutunza, basi hutoweza kutulia. Utafikiri kuwa ni jukumu lako kuhangaikia kila hitaji lako, kimwili, kihisia na hata kiroho. ¹
 - 1 Petro 5:7 Mwekeeni matatizo yenu yote, maana yeye anawatunzeni.
 - Zaburi 55:22 Mwachie Mwenyezi-Mungu mzigo wako, naye atakutegemeza; kamwe hamwachi mwadilifu ashindwe.

¹ Seeking God's Kingdom by David B. Curtis (<http://www.bereanbiblechurch.org>)

(b) Amini

- ❑ “Ilishe imani yako na tazama mashaka yako yakifa kwa njaa.” wasiwasi ni njia itokayo mahali ulipo na kukupeleka usipopajua; usiiruhusu iongoze maisha yako. Hofu ya siku zijazo ni kupoteza ya leo.¹
- ❑ Mwinjilisti Billy Sunday alisema, “hofu iligonga mlango wangu, Imani iliitikia.. Na hakukuwa na mtu tena.”
- ❑ Usiwe na wasiwasi kuhusu kesho, MUNGU ameshafika!



Billy Sunday (1862–1935)

¹ <http://junialeigh.wordpress.com>

(c) Sifu


□ Sifu

➤ Habakuki 3:17-19 Hata miti isipochanua maua, wala mizabibu kuzaa zabibu; hata kama mizeituni isipozaa zeituni, na mashamba yasipotoa chakula; hata kama kondoo wakitoweka zizini, na mifugo kukosekana mazizini, mimi nitaendelea kumfurahia Mwenyezi-Mungu nitamshangilia Mungu anayeniokoa.

□ Kwa maneno mengine, hata kama hakuna mazao na uchumi umeshuka, usiwe na wasiwasi - msifu Mungu - naye " atakupitisha juu ya milima."

(d) Kubali

- Walipo hukumiwa kuteketea katika tanuri la moto, marafiki wa Danieli katika kauli yao kwa Nebukadreza walisema sio tu uwezo wa Mungu kuwaokoa bali uhuru kamili atakaowapa.
- Danieli 3:16-18 Shadraki, Meshaki and Abednego wakamjibu mfalme, "... Ikiwa ndivyo, Mungu wetu ambaye tunamtumikia anaweza kutuokoa katika tanuri la moto mkali; tena atatuokoa mikononi mwako ee mafalme. Lakini, hata kama haitafanyika hivyo, ujue wazi, ee mfalme, kwamba sisi hatutaitumikia miungu yako.



2) MFUMO WA THAMANI

- Yesu hutufundisha kwamba Mungu hataki watoto wake wajishughuliche sana na starehe, na mambo ya mpito ya dunia.
- Mathayo 6:32-33 Maana hayo yote yanahangaikiwa na watu wasiomjua Mungu. Baba yenu wa mbinguni anajua kwamba mnahitaji vitu hivyo vyote. Bali shughulikieni kwanza ufalme wa Mungu na matakwa yake, na hayo yote mtapewa kwa ziada.

2) MFUMO WA THAMANI

- Hatutakiwi kutia shaka sana bali mwenendo wetu kwa Mungu. Biblia inatuambia kwamba sisi si watu wa dunia bali raia wa mbinguni.
 - Wafilipi 3:19-20 ...hufikiria tu mambo ya kidunia. Lakini sisi ni raia wa mbinguni.
 - Waebrania 13:14 Maana hapa duniani hatuna mji wa kudumu; lakini tunautafuta ule unaokuja.

2) MFUMO WA THAMANI

- ❑ Tunatakiwa kuelewa kwamba tofauti na wanyama, binadamu wameumbwa kwa mfano wa Mungu.
 - Mwanzo 1:7 Basi Mwenyezi-Mungu akamuumba mwanamume kwa mavumbi ya udongo, akampulizia puani pumzi ya uhai, na huyo mwanamume akawa kiumbe hai.
- ❑ Mungu hujali wanyama pia, lakini binadamu ni taji la uumbaji wake na ni wanaopendelewa zaidi.
 - Mathayo 6:26 "Waangalieni ndege wa mbinguni... Je, nyinyi si wa thamani kuliko hao?"
- ❑ Hakuna ndege au mnyama yeyote mwenye kuungana na urithi wa Yesu Kristo. Hakuna ndege ambaye ametakaswa na Mungu. Hivyo kama Mungu huwajali na kuwatunza ndege, hudhani kwamba atakujali?

2) MFUMO WA THAMANI

- “Je, maisha ni chakula tu au zaidi? Na mwili, je, si zaidi ya mavazi?” (Mathayo 6:25)
- Watu wengi leo hupima thamani ya maisha kwa vitu vinavyowazunguka. Huweza kuonekana ni vya kudumu au vyenye thamani, lakini kiuhalisia ni vya muda tu... kila tunachokimiliki huweza kupotea ndani ya muda mchache tu. Kwa kuongezea, vitu ambavyo huweza kununuliwa kwa pesa vina umuhimu mdogo, ukilinganisha na vitu ambavyo pesa haiwezi kununua... familia, upendo, marafiki na vingine muhimu kama uadilifu, uaminifu, uvumilivu, huruma na ukarimu. Hivi hupaswa kuwa muhimu sana kwetu hupaswa kuwa muhimu sana kwetu kuliko vitu. Maisha si vitu. TUSIRUHUSU vitu viendeshe mawazo yetu. ¹

¹ <http://christianlives.org/sermons/ANXIETY86.doc>

2) MFUMO WA THAMANI


- ❑ Kama utakuwa na mtazamo wa Kimungu hutatafuta ushauri sehemu tofauti. (yaani ushauri wa kisaikolojia)
 - Zaburi 2:1 Heri mtu yule ambaye haendi katika shauri la watu waovu...
- ❑ Ayubu husema kuhusu Mungu kwamba, "Yeye anayo mashauri na ufahamu." (Ayubu 12:13)
- ❑ Yesu aliita "Mshauri wa Ajabu" (Isaya 9:6).
- ❑ Na Yesu alisema juu ya Roho Mtakatifu ambaye hukaa ndani yetu, "Nami nitamwomba Baba, naye atawapeni Msaidizi mwingine akae nanyi siku zote." (Yohana 14:16)



2) MFUMO WA THAMANI

- ❑ Wakati wengine wakijaribu na kuunganisha mashauri ya kikristo na kisaikolojia, zingatia watu hawa wawili mashuhuri ambao maneno yao yameunda saikolojia ya sasa
- ❑ Freud alipinga Ukristo na alisema kwamba mafundisho ya dini ni udanganyifu na kwamba dini ni "ugonjwa wa akili kwa walimwengu." Aliona dini ni kama chanzo cha matatizo ya akili na mwishowe kuandaa dhana zake za kutomcha Mungu.¹

¹ CHANZO: <http://www.psychoheresy-aware.org/jungleg.html>



Sigmund Freud
(1856–1939)


2) MFUMO WA THAMANI

- Kitendo cha kutokukubaliana kati ya Freud na Jung kilitokana na "Jung kujitolea katika dini, kitu ambacho Freud aliona si cha kisayansi." ¹
- Jung alijiingiza ndani zaidi na kuwa na mawasiliano ya kila siku na roho wasioonekana, ambao aliwaita 'archetypes'. Makala nyingi alizoandika zilitawaliwa na vitu hivyo. Jung alikuwa na roho wake ambaye alimwita Philemon ambaye aliandika juu yake kwamba, "Nilikwenda naye tukitembea bustanini, na kwangu alikuwa kama yule ambaye Wahindi humwita guru."³

¹ Wikipedia - Sigmund Freud

² SOURCE: <http://www.psychoheresy-aware.org>


³ Jung, Memories, Dreams, Reflections



Carl Jung
(1875–1961)

2) MFUMO WA THAMANI

- Saikolojia ya Kibinadamu imechangia kwa kiasi kikubwa kuufanya ulimwengu huu uamini katika 'ubinafsi' na iliendelezwa na Abraham Maslow na Carl Rogers.. Mawazo ya Maslow juu ya maendeleo ya binadamu katika muongozo wa mahitaji yana tofauti kubwa na mahubiri ya Yesu pale mlimani. Yesu anasema kwamba, wasiomjua Mungu ndiyo huangaika na hayo : "tutakula nini" na "tutakunywa nini". Lakini Yesu anasema, "utafuteni kwanza Ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." (Mathayo 6:33)



¹ <http://procinwarn.com/building.htm>

2) MFUMO WA THAMANI

- Na Yesu alisema Roho Mtakatifu atakuwa Mshauri wetu, atatufanya tuwe na amani na mioyo yetu isiwe na shaka (tusiwe na dukuduku).
 - "lakini Msaidizi, Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, atawafundisheni kila kitu na kuwakumbusheni yote niliyowaambieni. Nawaachieni amani; nawapeni amani yangu. Siwapi nyinyi kama vile ufanyavyo. Msiwe na wasiwasi, wala msifadhaike." (Yohane 14:26-27)
- Kama unahitaji ushauri, AIDHA;
 - Tafuta uso wa Mungu kwa maombi na kwa Neno la Mungu. AU
 - Mpate mtu aliyejazwa Roho Mtakatifu akushauri - kwa uongozi wa kanuni za Biblia, na sio saikolojia ya kibinadamu.

2) MFUMO WA THAMANI

- Mtazamo wa Kimungu huingia vipi katika maeneo matatu yanayopelekea msongo wa mawazo ambayo Yesu aliyatoa kama mfano?
 - a) Chakula (mahitaji muhimu)
 - b) Nguo (mitindo)
 - c) Maisha marefu (afya)

(a) Mahitaji muhimu

- Mtazamo wa Kimungu huelewa kwamba Mungu ni Baba yetu naye atatupatia;
 - Tusiwe na shaka kwani kuna mengine mengi katika maisha kuliko vitu. Aliongelea kuhusu watu kuwa na shaka juu ya chakula, mavazi na urefu wa maisha. Anawakumbusha maisha ni zaidi ya chakula na mwili zaidi ya mavazi. Kwa kuongezea, kwa kuwa wasiwasi hakuna mtu miongoni mwetu anaweza kuongeza siku moja katika maisha yake. Kwa maneno mengine wasiwasi haufanikishi kwa sababu maisha ni zaidi ya kidunia. ¹

¹ <http://christianlives.org/sermons/ANXIETY86.doc>

(b) Mitindo

- Mtazamo wa Kimungu unaelewa kwamba sio mavazi ya kimitindo, lakini tabia ndiyo hubeba uzuri wa kweli.
 - 1 Petro 3:3-5 Katika kujipamba kwenu msitegemee mambo ya nje nje, kama vile mitindo ya kusuka nywele, kujivalia vitu vya dhahabu na nguo maridadi. Bali, uzuri wenu unapaswa kutokana na hali ya ndani ya utu wa kweli, uzuri usioharibika wa wema na utulivu wa roho, ambao ni wa thamani kubwa mbele ya Mungu. Ndivyo walivyojipamba hapo kale wanawake waadilifu waliomtumainia Mungu.
- Tukiwa tunatumia nguvu nyingi ili kuonekana vizuri, Yesu hutuonesha maua ya porini - ambayo yamevikwa vizuri na Mungu - yana uzuri mno.

- ❑ Yesu alisema kwamba pamoja na utajiri wa Mfalme Suleiman hakuwa na vazi ambalo linafanana na uzuri wa maua ya porini. Mungu ambaye hupendezesha maua atawapatia mavazi muhimu watoto Wake.
- ❑ Hivyo kwa nini tunapoteza nguvu zetu juu ya hayo? Yesu anatufundisha kwamba nguvu zetu zielekee kuutafuta Ufalme wa Mungu kama pendeleo letu la kwanza.



(c) Afya na Maisha marefu

- ❑ Swali: Je, chakula muhimu ni kupoteza muda na mazoezi ni bure?
- ❑ Jibu: Hapana, Paulo husema katika Wafilipi 3:19 kwa ambao “tumbo lao ndilo mungu wao” Biblia huwapa tahadhari kwa tamaa yao. Kufunga kumepewa ruhusa na Biblia. Kuna faida ya mazoezi (kwa maisha ya sasa).
 - 1 Tim 4:7-8 Lakini... Jizoeshe kuishi maisha ya uchaji Mungu. Mazoezi ya mwili ya faida yake, lakini mazoezi ya kiroho yana faida za kila namna, maana yanatuahidia uhai katika maisha ya sasa, na pia hayo yanayokuja.
- ❑ Mtazamo wa Kimungu hutambua kwamba, kwa kufanya mazoezi ya kukimbia na kuzunguka jengo kila siku huwezi kumlazimisha Mungu akuache uishi zaidi. Mungu huamua urefu wa maisha yako na atakuacha hai kwa muda alioupanga.



3) MARA MOJA KWA SIKU

- ❑ Usiishi katika ulimwengu wa kufikirika wa "itakuwaje?".. Itakuwaje kama hili au lile likitokea?
- Itakuwaje lisipotokea? Hatakama likitokea, unaweza kukabiliana nalo. Yesu alisema kwamba, "Matatizo ya siku moja yanawatosheni kwa siku hiyo."(Mathayo 6:34)
- Shughulikia matatizo ya leo katika siku ya leo na uyaache matatizo ya kesho kwa ajili ya kesho. Yesu anatuelekeza. "Msiwe na wasiwasi juu ya kesho; kesho ina yake." (Mathayo 6:34)

3) MARA MOJA KWA SIKU



3) MARA MOJA KWA SIKU



3) MARA MOJA KWA SIKU

- ❑ "Tutafanikiwa endapo tutachukua hatua ya kubeba mzigo wa siku husika, lakini mzigo utakuwa mzito zaidi kwetu kama tutabeba mzigo wa jana katika siku ya leo na tena kuongezea mzigo wa kesho kabla hatujalazimika kuubeba."
(John Newton)
- ❑ Mcheshi na Mtumishi wa Kanisa, Robert Jones Burdette alisema, "Kuna siku mbili katika wiki ambazo sizijali sana... jana na kesho."

Maamuzi ni yetu. Tunaweza kuchagua kuchukua matatizo ya kesho na kuishi kama Mungu hayuko, au tumwamini Yeye na kumtafuta kwa moyo wote.

3) MARA MOJA KWA SIKU

- Yesu anatuambia tusiwe na wasiwasi kwa sababu tunaishi mara moja kwa siku. Kwa maneno mengine, tunaishi katika wakati huu - leo. Hii ni dhahiri, lakini halina maana kwa wengi. Wanajua kesho inakuja na huamua kuitilia wasiwasi.¹
- Yesu alisema: "Njoni kwangu nyinyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mkajifunze kwangu, maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtatulizwa rohoni mwenu. Maana, nira niwapayo mimi ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." (Mathayo 11:28-30)

**Amua kuishi leo. Igeuze kesho
kwa Mungu.**

¹ Ibid

NAWAPENI AMANI

- Yesu pia alisema:
 - “Nimewaambieni mambo haya ili mpate kuwa na amani katika kuungana nami. Ulimwenguni mtapata masumbuko; lakini jipeni moyo! Mimi nimeushinda ulimwengu!” (Yohane 16:33)
 - “Nawaachieni amani; nawapeni amani yangu. Siwapi nyinyi kama vile ulimwengu ufanyavyo. Msiwe na wasiwasi, wala msifadhaike.” (Yohane 14:27)
- Yesu hatupi amani kama ulimwengu ufanyavyo kwa sababu yeye ni “Mfalme wa Amani” (Isaya 9:6).
 - **Amani ya kweli yatoka ndani** – sio nje, hutegemeana na hali ya nje. Unaweza kuwa na Amani ya kweli ya Yesu katika shida.

Audio (WMA) and text (PDF) ministry

FREE MINISTRY DOWNLOADS



MWANDISHI:
Gavin Paynter

IMETAFSIRIWA NA:
Francis Gabriel Bwire Masome

- <http://www.agfbenoni.co.za/ministry-archives.aspx?speaker=SWAHILI>